**IN THE HIGH COURT FOR ZANZIBAR**

HOLDEN AT VUGA

CIVIL APPEAL NO. 38 OF 2012

FROM ORIGINAL APPLICATION NO. 26 OF 2012

OF THE LIQUOR BOARD AT MWANAKWEREKWE ZANZIBAR

LUKENGE BAR (MPENDAE) --------- APPELLANT

***V E R S U S.***

1. ABDALLA MNUBI
2. HASSAN BAKAR SULEIMAN
3. KHALIB AHMADA OMAR -------- RESPONDENT

---

*Tarehe ya Amri ya Mwisho: 1/10/2012*

*Tarehe ya Hukumu: 24/10/2012.*

**HUKUMU**

**RABIA H. MOHAMED, J.**

Muomba rufaa, Lukenge Baa (Mpendae) ameleta rufaa yake hii baada ya kutoridhika na hukumu na amri ya Mahkama ya Leseni ya Vileo iliyokaa na kutoa uamuzi wake tarehe 11 May 2012. Awali Muomba rufaa aliwasilisha ombi mbele ya Mahkama hiyo kwa ajili ya kupatiwa leseni ya biashara ya vileo ya mwaka 2012.

Waombewa Rufaa ni Abdalla Mnubi, Hassan Bakari Suleiman na Khalid Ahmada Omar ambao awali walikuwa ni Wapinga Ombi.

Muomba Rufaa amejiwakilisha mwenyewe mahkamani hapa na Waombewa Rufaa wamewakilishwa na wakili msomi Suleiman Salim.

Muomba Rufaa ameleta sababu sita za rufaa kama ifuatavyo:-

1. Kwamba Mheshimiwa Mwenyekiti wa Mahkama ya vileo amepotoka kisheria kwa kuendesha kikao maalum chini ya kifungu cha 60 (1) (2) cha Cap 163 na kukitumia kumnyima muombaji leseni kwa mwaka 2012.

2. Kwamba Mheshimiwa Mwenyekiti wa Mahkama ya vileo amepotoka kisheria kwa kuendesha kikao maalum (special meeting) chini ya kifungu cha 60 (1) (2) cha Cap 163 na kufikia kutoa maamuzi ya kumnyima muombewa leseni kwa mwaka 2012, bila ya kukitangaza kikao hicho kwenye gazeti la Serikali kama inavyotakiwa na Sheria.

3. Kwamba Mheshimiwa Mwenyekiti wa Mahkama ya vileo amepotoka kisheria kwa kuitisha, kuendesha kikao maalum chini ya kifungu cha 60 (1) (2) cha Cap 163 na kukitumia kutoa/kukataa na kurenew

leseni za kila mwaka na kufikia kumnyima muombaji leseni kwa mwaka 2012, kinyume na matakwa ya Sheria ya Vileo Cap 163.

4. Kwamba Mheshimiwa Mwenyekiti wa Mahkama ya vileo amepotoka kisheria kwa kuzingatia maelezo yasiyothibitishwa ya waombewa rufaa na 1, 2 na 3 ambayo wajumbe wake wameyatumia kumshawishi kumkatalia muomba rufaa kupewa kibali cha kukata leseni 2012.

5. Kwamba Mheshimiwa Mwenyekiti wa Mahkama ya vileo amepotoka kisheria kwa kutoa maamuzi ya kumnyima muombaji leseni kwa sababu ya wakaazi na majirani wa karibu sana Sheria 163 kifungu 60 (c) hawataki kuwepo Bar eneo hilo, ikiwa hakuna jirani mmoja wa karibu aliepinga ila wapingaji wote ni wakutoka mbali.

6. Kwamba Mheshimiwa Mwenyekiti wa Mahkama ya vileo amepotoka kisheria kwa kutoa maamuzi ya kumnyima muombaji leseni kwa kuzingatia maoni ya wajumbe wa Bodi ambayo hayana sababu

zinazokubalika na Sheria za muombaji kukataliwa kupewa leseni.

Katika kuelezea sababu ya kwanza ya rufaa Muomba rufaa aliieleza Mahkama kuwa Mahkama ya leseni ya vileo ilienda kinyume na taratibu kwa kuendesha kikao chini ya kifungu cha 60 (1) (2) Sura ya 163, na pia ilipitiliza muda unaotakiwa kufanya kikao chake.

Baada ya hapo Muomba rufaa alizitaja sababu yake ya pili na ya tatu za rufaa kama zilivyo katika hati yake ya rufaa.

Nae Wakili msomi Suleiman Salim aliyewawakilisha waombewa rufaa namba 1, 2 na 3 alipinga rufaa hii na alijibu sababu ya kwanza, pili na ya tatu ya rufaa kwa pamoja kwa kutoa majibu ya hoja ambayo hayakuiridhisha Mahkama hii. Pengine alijisahau kwamba yeye ni afisa wa Mahkama ambae wajibu wake ni kuisaidia Mahkama ili ifikie maamuzi sahihi. Hoja za Muomba rufaa zilijibiwa na Wakili msomi Suleiman Salim kama kwamba aliyekuwa anatoa majibu hayo ni mtu asiye mtaalam (layman). Wakili msomi Suleiman Salim alijibu sababu hizi tatu za rufaa kwa kueleza kuwa kama Muomba rufaa anasema kuwa Mahkama ya leseni ya vileo haikuwepo kisheria ni vipi basi alipeleka ombi lake la kupatiwa leseni ya biashara ya vileo. Kuhusu sababu ya rufaa kwamba Mahkama ya leseni ya vileo ilafanya kikao chake bila ya kukitangaza kikao hicho kwenye gazeti rasmi la Serikali, wakili msomi Suleiman Salim alieleza kwamba tangazo hilo lilitoka na uthibitisho wa hili ni

kitendo cha muomba rufaa kufika katika Mahkama ya leseni ya vileo tarehe ya kusikilizwa ombi na kwamba Muomba rufaa alipaswa kutafuta magazeti yote ya Serikali na kwa kuithibitishia Mahkama kwamba tangazo hili halikutoka. Alimalizia katika kujibu sababu hizi tatu za rufaa kwa kueleza kwamba Order VIII Rule 2 ya Sheria ya Mwenendo wa Madai inawataka wadaawa kwenye kesi kutoa hoja zao juu ya uhalali wa Mahkama siku ya kwanza ya kusikilizwa kesi.

Kabla ya kuendelea na maelezo ya sababu ya nne, tano na sita za rufaa hii, Mahkama imeona ianze kutolea uamuzi hoja zilizotolewa na pande zote mbili za rufaa katika sababu ya kwanza, pili na ya tatu.Kifungu cha 60 (1) (2) cha Sura ya 163 ambacho ndio msingi wa sababu ya kwanza, pili na tatu za rufaa hii kinasomeka kama ifuatavyo: -

> *"60 (1) A special meeting of the licensing court may be held, subject to three weeks' notice thereof being published in the Gazette, and the posting of notices referred to in section 62, on the application of any person desirous of obtaining an* ***interim licence*** *upon payment of a fee of forty-five shillings.*

*(2) Any licence granted at any special meeting of the licensing court shall continue in force only until the close of its annual meeting."*

Kifungu hichi cha 60 Sura ya 163 kinahusiana na maombi ya leseni za muda ambao utaratibu wa kufanya maombi hayo umeelezewa katika vifungu vya 61 na 62 vya Sura ya 163. Suali ninalojiuliza hapa ni leseni gani ya vileo aliyoomba Muomba rufaa katika kikao cha Mahkama hii cha mwezi May 2012 ambayo ndio chanzo cha rufaa hii.

Kifungu cha 61 cha Sheria ya Vileo Sura ya 163 kinatoa maelekezo kwa muombaji kufanya ombi la leseni kwa kujaza moja katika fomu zitakazotolewa kwa niaba hiyo. Kifungu hichi kinasomeka kama ifuatavyo: -

*"61. Any person desiring to obtain a licence or a renewal thereof for the sale of liquor under this Decree (save and except where otherwise provided for), or the transfer of a licence by the holder thereof to any other person, or the removal of any other premises, shall make application on one of the forms prescribed in that behalf, in triplicate, to the licensing officer not later than seven days after the date of the publication of the notice referred to in section 45."*

Katika kupitia kumbukumbu za ombi la muombaji ambalo ndio chanzo cha rufaa hii Mahkama hii imekuta fomu ambayo imejazwa ina jina la muomba rufaa na eneo ilipo biashara husika tu, licha ya kwamba fomu hii ina taarifa kumi na tatu na vipengele ndani yake viinavyotakiwa kujazwa na Muomba rufaa na wahusika wengine wa ngazi mbali mbali za Serikali. Taarifa kumi na mbili kati ya hizi hazikuwa zimejazwa kabisa, na katika taarifa ya kwanza imejazwa pungufu ambapovimejazwa vipengele viwili tu nilivyovitaja hapo juu kati ya vipengele tisa vinavyopaswa kujazwa.

Mahkama hii haikuishia hapo, niliangalia mwenendo wa kesi ambapo tarehe 3 May 2012 Mahkama ya Leseni ya Vileo ilikaa na kusikiliza ombi la muomba rufaa ambapo maelezo ya muomba rufaa/ muombaji yalikuwa kama ifuatavyo: -

**MAELEZO YA MUOMBAJI**

**JINA: SAIMON BENEDICT KUNAMBI MIAKA 48 NAISHI MPENDAE DINI CHRISTIAN AMEAPA NA KUSEMA:**

Mimi naiombea bar ya Lukenge bar iliyopo Mpendae mimi ndio mmiliki wa bar hiyo, hivyo naomba kupatiwa leseni ya kuuzia vileo ya mwaka 2012. Mimi nalipa kodi zote za Serikali pamoja na kujiajiri mwenyewe.

Sgd: Omar M. Hamza

Mwenyekiti

3/5/2012

Katika rufaa hii kumbukumbu za Mahkama hazioneshi kwamba Muomba rufaa alifanya ombi mbele ya Mahkama ya Leseni ya Vileo. Hii ni kwa sababu hakuwa amejaza fomu kama matakwa ya kifungu cha 61 Sura 163 yanavyoelekeza. Nitakuwa sahihi kusema kwamba katika rufaa hii iliyotokana na ombi la leseni ya vileo, muomba rufaa hakuwa amefanya ombi kabisa, si la leseni ya mpito wala leseni nyengine ya biashara ya vileo ya mwaka 2012 kinyume na maelezo yake yanavyosomeka hapo juu. Sielewi ni kwa vipi Mahkama ya leseni ya vileo ilikaa na kusikiliza ombi hilo na hata kufikia kutoa maamuzi ambayo ni chanzo cha rufaa hii.

Kufikia hapa basi na kutokana na sababu nilizozieleza hapo juu Mahkama hii haioni sababu ya kuendelea kujadili sababu nyengine za rufaa hii na hivyo rufaa inatupiliwa mbali. Gharama kwa muomba rufaa.

Sgd: Rabia H. Mohamed

Jaji

24/10/2012.

**Court:** Hukumu imesomwa leo tarehe 24 October, 2012, mbele ya Muomba Rufaa na Mpinga Rufaa.

Sgd: Rabia H. Mohamed

Jaji

24/10/2012.

**Nathibitisha kuwa hii ni Nakala Halisi ya Hati ya Asili.**

Sgd. **GEORGE J. KAZI**

MRAJIS

MAHKAMA KUU

**Z A N Z I B A R.**